Koksidiosis (Kuhara damu)

Huathiri kuku wa rika zote lakini huua zaidi vifaranga na kuku wanaokua hasa kati ya wiki ya kwanza hadi ya nne.

Dalili

- Kinyesi cha rangi ya kahawia au kilichochanganyika na damu.
- Manyoya kuvurugika na kushusha mabawa (kuvaa koti).

Kinga na tiba

- Kuku wapewe dawa ya koksidiosis wanapofikisha wiki moja.
- Kusafisha vyombo vya kuwekea maji mara kwa mara.
- Kuepuka unyevu ndani ya banda.
- Kuwapatia kuku dawa aina ya Amproliamu, Esb3, salfa au dawa ya koksidiosi utakayoelekezwa na mtaalam wa mifugo pale ugonjwa unapokuwa umejitokeza.

Minyoo

Minyoo hukaa tumboni mwa kuku na ikizidi husababisha kuku kupunguza kutaga, kupoteza uzito na hata kusababisha vifo kwa kuku.

Dalili

- Kuku kujidonoa sehemu ya haja kubwa.
- Minyoo kuonena katika kinyesi.

Kinga na tiba

Kuku wapewe dawa ya minyoo kama vile piperazine citrate kila baada ya miezi mitatu.

Ndui ya kuku (Fowl pox)

Huathiri zaidi vifaranga na kuku wanaokua, hutokea mara nyingi wakati wa mvua. Husababishwa na virusi wa ndui ya kuku.

Dalili

Vivimbe katika sehemu mbalimbali za mwili wa kuku zilizo wazi kama usoni, vishungi, kuzunguka mdomo, miguuni na

Jogoo mwenye ndui na kifaranga mwenye ndui.

Picha: Mtandao

Kinga na tiba

Ugongwa huu hauna tiba ila huzuiwa kupitia chanjo ya ndui kila baada ya miezi sita.

Imetayarishwa na:

Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI)
S.L.P 00100-30709, Nairobi, Kenya.
Simu: +254·20·422·3000
E·mail: b.lukuyu@cgiar.org

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)
West Kilimanjaro,
S.L.P 147 Sanya Juu, Moshi, Tanzania
Simu +255 784 705 134
E-mail: l.marwa@cgiar.org

Toleo hili limefanikishwa kwa msaada wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia mradi wa Utafiti wa kilimo endelevu kwa ajili ya kizazi kijacho Afrika (Africa RISING) kama sehemu ya mpango wa serikali ya Marekani wa Feed the Future.

www.africa-rising.net

Magonjwa muhimu ya kuku wa asili



Picha: Mtandao

Magonjwa ya kuku ni chanzo kikubwa cha hasara kwa mfugaji. Kugundua dalili za ugonjwa ni hatua muhimu kwa mfugaji ili kupata tiba sahihi kabla ya kuku kuzidiwa. Lishe bora, usafi wa banda na vyombo vya kuwekea maji na vyakuka hupunguza kutokea kwa magonjwa. Chanjo hupunguza gharama za tiba na hasara itokanayo na kutokutaga au vifo kwa kuku wagonjwa.

Dalili za jumla kwa kuku mgonjwa

- Mchovu na dhaifu, hupenda kukaa na kulala au kusimama akiwa amejikunja.
- Macho yasiyong'aa na sura iliyosinyaa.

- Rangi ya upanga kufifia.
- Hula na kunywa maji kidogo kuliko kawaida.
- Huwa na manyoya yaliyovurugika na yenye kunyonyoka kwa urahisi.
- Kinyesi kisichokuwa cha kawaida na Sehemu ya kutolea haja inakuwa na unyevunyevu na kinyesi kuganda.
- Hupumua kwa sauti, kukohoa, kupiga chafya au kutokwa na kamasi.
- Huwa na tabia ya kujitenga na wenzake katika kundi.
- Kuku hukonda.
- Hupunguza kutaga au husimama kutaga kabisa.

Yafuatayo ni magonjwa ambayo huongoza katika kusababisha vifo vya kuku wa asili.

Mdondo/ Kideri (Newcastle)

Unasababishwa na virusi wa mdondo. Huathiri kuku wa rika zote na huweza kuua kuku wengi hata 100% kwa wakati mmoja.

Dalili

1. Kuharisha kinyesi cha kijani au chenye mchanganyiko wa rangi ya njano.
2. Kupooza miguu, mabawa, na hujizungusha mahali alipo au huzungusha kichwa na kutembea kinyumenyume.
3. Kupumua kwa shida.
4. Kutoa kamasi na kupiga chafya.

Uchunguzi wa mzoga

Ugonjwa huathiri zaidi mfumo wa hewa na njia ya chakula. Unafanya mzoga unakuwa na:

- Madoa ya damu kwenye mfumo wa hewa.
- Kamasi nzito zenye rangi ya njano kwenye koromeo.
- Utandu mweupe kwenye mifuko ya hewa.
- Bandama kuvimba.
- Uvimbe kwenye kichwa na eneo la shingo.
- Madoa madogo madogo ya damu kwenye kifua, mafuta na utandu wa tumboni.
- Damu kuvia kwenye mfumo wa usagaji chakula- juju, firigisi, tumbo na utumbo.

Filigisi iliyovia damu.

Picha: Mtandao

Tiba na kinga

Ugonjwa huu hauna tiba ila huzuiwa kupitia chanjo ya mdondo wiki ya kwanza kwa vifaranga, irudiwe baada ya wiki moja na baadaye ifanyike kila baada ya miezi mitatu.

Homa kali ya matumbo (Fowl Typhoid)

Ugonjwa huu unasababishwa na bacteria na hushambulia rika zote za kuku.

Dalili

- Kuharisha kinyesi cha majimaji na cha rangi ya njano/ nyeupe.
- Vifaranga wanatotolewa wakiwa wamekufa au dhaifu.
- Vifaranga hujikusanya pamoja na kukosa hamu ya kula.

Uchunguzi wa Mzoga

- Kinyesi cha rangi ya njano/nyeupe kwenye manyoya ya sehemu ya kutolea haja kubwa.
- Misuli iliyovia na damu kuwa nyeusi.
- Ini lililovimba na kuwa na rangi ya pinki.
- Bandama lililovimba.
- Figo na mayai yaliyovia.
- Mabaka meupe kwenye sehemu ya juu ya figo.

Tiba na kinga

Madawa aina ya antibaotiki, kwa mfano OTC.

Mafua ya kuku (Infectious Coryza)

Ugonjwa huu unasababishwa na bacteria ambao hushambulia zaidi kuku na ndege wa porini. Ugonjwa huu hushambulia zaidi mfumo wa hewa katika kuku wa umri wote.

Huambukizwa kupitia maji na chakula kilichochafuliwa na kinyesi cha kuku wagonjwa. Kuku au ndege wagonjwa huambukiza wenzao kupitia mfumo wa hewa wanapopiga chafya.

Dalili

- Uso mzima unavimba pamoja na upanga.
- Kuku anashindwa kupumua, hukohoa na kupiga chafya.
- Harufu mbaya kutoka kinywani na machoni.

Ukosefu wa vitamin A

Huathiri zaidi vifaranga na kuku wanaokua. Ugonjwa huu hujitokeza zaidi wakati wa kiangazi ambapo wadudu na majani mabichi ni machache. Kuku wafungiwao ndani wanapatwa zaidi na tatizo hili.

Dalili

Macho huvimba na kutoa uchafu mzito mweupe kama usaha ambao huganda kafanya mabonge meupe ndani ya jicho. Jicho huweza kuharibika na kusababisha upofu. Mara nyigi inatokea kwa jicho moja.

Tiba na kinga

Ugongwa huu huweza kuzuiwa kwa kuwapatia kuku dawa yenye vitamin A mfano vitalyte. Kwa kuku walioathirika, wapewe mara mbili hadi nne ya dozi ya vitamini iliyopendekezwa, iambatane na antibaotiki mfano OTC au Neoxy-vitamin. Matumizi ya majani au masalia ya mbogamboga yafaa sana kama chanzo cha vitamin.